# NATION MEDIA GROUP PLC

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA

Taarifa inatolewa hapa kuwa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Sitini na Mbili wa Wanahisa wa Nation Media Group PLC utafanyika kwa njia ya kielektroniki siku ya Ijumaa, tarehe 27 Juni 2025 kuanzia saa tisa alasiri EAT kwa ajili ya kujadili shughuli zilizoainishwa hapa chini.

*Maazimio yote yatafanyika kwa njia ya Kura ya Maoni.*

### SHUGHULI ZA KAWAIDA

**1.** Kupokea taarifa za kifedha za mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba 2024, pamoja na ripoti za Mwenyekiti, Wakurugenzi na Wakaguzi.

**2.** Kuelezwa kuwa Wakurugenzi hawapendekezi gawio kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba 2024.

**3.** Kupokea, kuzingatia na iwapo itafaa, kupitisha Ripoti ya Malipo ya Wakurugenzi na malipo yaliyolipwa kwa Wakurugenzi kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2024 na kuidhinisha Bodi kuweka viwango vya malipo kwa Wakurugenzi Wasio Wakuu.

**4.** Kuthibitisha kuwa Wakaguzi, PricewaterhouseCoopers LLP, ambao wameonesha nia ya kuendelea, waendelee kuwa Wakaguzi wa Kampuni kwa mujibu wa kifungu cha 721(2) cha Sheria ya Kampuni za Kenya, Sura ya 486, Sheria za Kenya na kuwaidhinisha Wakurugenzi kuweka malipo ya Wakaguzi kwa mwaka wa kifedha unaofuata.

**5.** Kuwachagua tena Wakurugenzi:
- a) Kwa mujibu wa Kifungu cha 96 cha Katiba ya Kampuni, Bi. Nancy Booker anastaafu kwa zamu na kwa kuwa ametimiza masharti, anajitolea kuchaguliwa tena;
- b) Kwa mujibu wa Kifungu cha 96 cha Katiba ya Kampuni, Bw. Paul Kasimu anastaafu kwa zamu na kwa kuwa ametimiza masharti, anajitolea kuchaguliwa tena;
- c) Kwa mujibu wa Kifungu cha 96 cha Katiba ya Kampuni, Bw. David C Nchimbi anastaafu kwa zamu na kwa kuwa ametimiza masharti, anajitolea kuchaguliwa tena;
- d) Kwa mujibu wa Kifungu cha 96 cha Katiba ya Kampuni, Bw. Joseph Muganda anastaafu kwa zamu na kwa kuwa ametimiza masharti, anajitolea kuchaguliwa tena;
- e) Kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Katiba ya Kampuni, Bw. Stephen Dunbar-Johnson anastaafu kwa zamu na kwa kuwa ametimiza masharti, anajitolea kuchaguliwa tena;
- f) Kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Katiba ya Kampuni, Bw. Louis Otieno anastaafu kwa zamu na kwa kuwa ametimiza masharti, anajitolea kuchaguliwa tena;
- g) Kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Katiba ya Kampuni, Prof. Samuel Sejjaaka anastaafu kwa zamu na hatawania kuchaguliwa tena;
- h) Dkt. Yasmin Jetha, kwa kuwa amefikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu na hatawania kuchaguliwa tena;
- i) Dkt. Wilfred Kiboro, kwa kuwa amefikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu na hatawania kuchaguliwa tena.

**6.** Kuwateua Wanachama wa Kamati ya Ukaguzi, Hatari na Utiifu ya Kampuni:

Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 769(1) cha Sheria ya Makampuni, Sura ya 486 ya Sheria za Kenya, Wakurugenzi wafuatao ambao ni wanachama wa Kamati ya Ukaguzi, Hatari na Utiifu ya Kampuni, wachaguliwe tena kuendelea kuhudumu kama wanachama wa kamati hiyo:
- a) Bw. David C Nchimbi
- b) Bw. Al-Noor Ramji

### SHUGHULI MAALUM

**7.** Kuipa Bodi Mamlaka ya Kutekeleza Majukumu Fulani:

Azimio lifuatalo lipitishwe kama Azimio la Kawaida:

Kuwa Bodi ipewe mamlaka ya kuandaa, kuidhinisha na kukagua mara kwa mara sera na taratibu zifuatazo kama inavyohitajika chini ya Kifungu cha 8.2 cha Ratiba ya Kumi na Tatu ya Kanuni za Masoko ya Mitaji (Matoleo ya Umma, Orodha na Ufichuzi wa Taarifa), ya mwaka 2023:
- **a)** Malipo
- **b)** Mawasiliano madhubuti na wanahisa na washikadau
- **c)** Sera na taratibu za ufichuzi wa taarifa za shirika
- **d)** Utatuzi wa migogoro ya ndani na ya nje
- **e)** Kuvutia na kuhifadhi wanachama wa Bodi

**8.** Shughuli nyingine yoyote ambayo Taarifa halali itakuwa imetolewa.

***Kwa Amri ya Bodi,***

Angela Namwakira
Katibu wa Kampuni

6 Juni 2025

### MAELEZO YA ZIADA:

1. Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Makampuni, Sura ya 486, Sheria za Kenya kama ilivyorekebishwa na Sheria za Biashara (Marekebisho) (Nambari ya 2), 2021, Mkutano Mkuu wa Mwaka (AGM) wa Sitini na Mbili wa Nation Media Group PLC ("Kampuni") utafanyika mtandaoni Ijumaa, Juni 27, 2025 saa tisa alasiri.
2. Wanahisa ambao wangependa kushiriki kwenye mkutano huo wanapaswa kujisajili mtandaoni kupitia https://digital.candr.africa/ au kwa kutumia USSD kwa kubonyeza *483*410# au kupitia kiungo kitakachotumwa kwao kupitia SMS na/au barua pepe na kufuata vidokezo mbalimbali kuhusu mchakato wa usajili. Ili kukamilisha usajili, wanahisa watahitajika kuwa na nambari yao ya Kitambulisho/Pasipoti iliyotumika kununua hisa zao pamoja na nambari yao ya akaunti ya hisa au CDSC.
3. Usajili wa Mkutano Mkuu wa Mwaka utafunguliwa tarehe 16 Juni 2025 saa tatu asubuhi na utafungwa tarehe 26 Juni 2025 saa sita mchana.
4. Kwa usaidizi, wanahisa wanaweza kupiga simu kupitia nambari zifuatazo: +254 20 8690360 kati ya saa mbili asubuhi hadi saa kumi unusu jioni wakati wa kipindi cha usajili. Wanahisa walioko nje ya Kenya wanapaswa kupiga nambari hiyo au kutuma barua pepe kwa: digital@candr.africa
5. Kwa mujibu wa Kifungu cha 283(2)(c) cha Sheria ya Kampuni, Sura ya 486, hati zifuatazo zinapatikana kwenye tovuti ya Kampuni: https://www.nationmedia.com
   - a. nakala ya Taarifa hii na Fomu ya Uwakilishaji;
   - b. Taarifa za Kifedha zilizokaguliwa za Kampuni kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba 2024.

6. Wanahisa ambao wangependa kuuliza maswali kabla ya Mkutano Mkuu wa Mwaka wanaweza kufanya hivyo kwa njia zifuatazo:
   - (i) Kupitia kiungo kitakachotumwa kwao kupitia sms au barua pepe baada ya kuthibitisha usajili; au
   - (ii) Kufikia Mkutano Mkuu wa Mwaka Mtandaoni kupitia https://digital.candr.africa/ au kupitia kiungo cha jukwaa la Mkutano Mkuu wa Mwaka; Chagua Attend Event; Chagua "Nation Media Group Plc AGM"; Chagua kichupo cha chaguo la "Q&A" na uwasilishe maswali katika kisanduku cha maandishi kilichotolewa; au
   - (iii) Kufikia Mkutano Mkuu wa Mwaka Mtandaoni kupitia jukwaa la USSD kwa kubonyeza *483*410#; Tumia vidokezo vya menyu ili Chagua chaguo la "Q&A" na uwasilishe maswali yako (ndani ya kikomo cha herufi 160 cha maandishi ya sms); au
   - (iv) Kutuma maswali kupitia barua pepe kwa digital@candr.africa ; au
   - (v) Ikiwa inawezekana, kupeleka maswali yaliyoandikwa wao wenyewe kwenye ofisi za Custody and Registrars Services Ltd, wasajili wa Kampuni, IKM Place, Ghorofa ya Kwanza, Tower B, 5th Ngong Avenue. Wanahisa wanaotuma maswali kupitia barua pepe au kuwasilisha kwa C&R Group sharti watoe maelezo yao kamili (majina kamili, Nambari ya Akaunti ya Hisa//Nambari ya Akaunti ya CDSC) wanapowasilisha maswali na ufafanuzi wao. Pia ambatisha nakala ya kitambulisho/Pasipoti yako.

   **MASWALI WAKATI WA MKUTANO**
   Wanahisa wataweza kuuliza maswali moja kwa moja kwenye jukwaa la mtandaoni la mkutano wa mwaka kwa kutumia jukwaa hilo la mtandaoni au msimbo wa USSD.

   **Maswali ya moja kwa moja wakati wa AGM**
   Kutakuwa fursa kwa wanahisa kujiunga na Mkutano Mkuu wa Mwaka (AGM) kwa njia ya mtandaoni ili kuuliza maswali yao wakati wa mkutano. Wahisa ambao wangependa kuuliza maswali yao moja kwa moja wakati wa AGM wanaweza kujiunga na chumba pepe cha mkutano (kwa kubofya sehemu iliyoandikwa "Join AGM Meeting Room" chini ya dirisha la maonyesho ya moja kwa moja). Katika chumba pepe cha mkutano, wanahisa wataendelea kutazama maonyesho ya AGM na wanaweza: i) kuchagua chaguo la "raise hand" kwenye skrini yao ili kuomba fursa ya kuuliza maswali yao moja kwa moja kwa Bodi; au ii) kuandika maswali yao kwenye sehemu ya mazungumzo ya moja kwa moja (live chat) ili yasomwe kwa Bodi wakati wa mkutano.

7. Wanahisa ambao wangependa kupiga kura wanaweza kufanya hivyo kwa:

8.
   - (i) Kufikia Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Mtandaoni kupitia https://digital.candr.africa/ au kupitia kiungo cha jukwaa; Chagua Attend Event; Chagua "Nation Media Group Plc AGM"; Chagua kichupo cha "Voting" na upige kura; au
   - (ii) Kufikia Mkutano Mkuu wa Mtandaoni kupitia USSD kwa kubonyeza 483410#; Fuata vidokezo vya menyu na uchague chaguo la "Voting" kisha ufuate vidokezo mbalimbali vya kupiga kura.

9. Kulingana na Kifungu cha 298(1) cha Sheria ya Kampuni, Sura ya 486, wanahisa wenye haki ya kuhudhuria na kupiga kura katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wana haki ya kuteua mwakilishi wa kupiga kura kwa niaba yao. Mwakilishi haitajiki kuwa mwanachama wa Kampuni lakini ikiwa hayupo, Mwenyekiti wa AGM atakuwa mwakilishi kwa chaguo msingi. Fomu ya uwakilishi imeambatishwa kwenye Taarifa hii na inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni https://www.nationmedia.com. Nakala halisi za fomu ya uwakilishi pia zinapatikana katika anwani ifuatayo:

   **Ofisi za Custody and Registrars Services,**
   **IKM Place, Tower B, 1st Ghorofa ya kwanza,**
   **5th Ngong Avenue.**

   Ili fomu ya uwakilishi iwe halali, sharti ijazwe kikamilifu na mwanahisa au wakili wake aliyeidhinishwa kwa njia ya maandishi. Ikiwa mwanahisa ni shirika, hati za kumteua mwakilishi zinapaswa kutiwa sahihi chini ya muhuri wake rasmi (ikiwa upo) au chini ya sahihi ya afisa au wakili aliyeidhinishwa wa shirika hilo.

   Fomu ya uwakilishi iliyojazwa kikamilifu inapaswa kutumwa kupitia barua pepe kwa proxy@candr.africa katika muundo wa pdf au iwasilishwe kwa Custody and Registrars Services, IKM Place, Tower B, Ghorofa ya Kwanza, 5th Ngong Avenue, Nairobi au kutumwa kupitia posta kwa Custody and Registrars Services, S. L. P. 8484-00100 Nairobi ili ifike kwa Msajili au Katibu wa Kampuni kabla ya saa tisa alasiri tarehe 26 Juni 2025.

   Fomu zilizojazwa kikamilifu sharti ziambatishwe na nakala ya Kitambulisho/Pasipoti halali ya mwanahisa pamoja na maelezo ya Kitambulisho/Pasipoti, anwani ya baruapepe au nambari ya simu ya mwakilishi ili kuwezesha usajili. Mawasiliano yatafanywa kwa mwanahisa yeyote husika ikiwa uwakilishi wake utakataliwa kabla ya saa kumi na moja jioni tarehe 26 Juni 2025 ili kutoa muda wa kushughulikia suala lolote lililojitokeza.

10. Mkutano Mkuu wa Mwaka utaonyeshwa moja kwa moja kwa wanahisa wote ambao watakuwa wamejisajili kushiriki katika mkutano mkuu.
11. Wanahisa na wawakilishi waliosajiliwa ipasavyo watapokea ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) na/au baruapepe saa mbili kabla ya kuanza kwa AGM, ukiwakumbusha kuwa mkutano utaanza baada ya saa mbili na ukitoa kiungo cha maonyesho ya moja kwa moja.
12. Wanahisa na wawakilishi waliosajiliwa ipasavyo wataweza kupiga kura (wakiombwa na Mwenyekiti) kupitia USSD kwa kubonyeza *483*410# au kupitia Jukwaa la Mkutano Mkuu wa Mwaka.
13. Kura ya maoni itafanywa kwa maazimio yote yaliyowasilishwa katika taarifa hii.

14. Matokeo ya AGM yatachapishwa kwenye tovuti ya kampuni (www.nationmedia.com) ndani ya saa 24 baada ya kukamilika kwa mkutano.

   Kwa migawio yoyote isiyodaiwa, njia inayopendekezwa ya malipo ya chini ya KShs 250,000 ni kupitia M-PESA. Wanahisa ambao wangependa kupokea migawio yao kupitia M-PESA na ambao hawajajisajili kwa njia hii ya malipo wanaweza kuchagua kupokea migawio ya baadaye kwa kubonyeza *483*038# au kuwasiliana na Msajili wa Hisa, Custody & Registrars Services Limited.

   Wanahisa wote wa sasa na wa awali wa Kampuni wanaarifiwa kuwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Mali za Kifedha Zisizodaiwa Nambari 40 ya mwaka wa 2011 Sehemu ya II na III, migawio na hisa ambazo hazijadaiwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) au zaidi zitakabidhiwa kwa Mamlaka ya Mali za Kifedha Zisizodaiwa ('Mamlaka') kama mali zilizotelekezwa katika tarehe iliyowekwa.

   Hivyo basi, wanahisa wote wa sasa na wa awali wenye migawio ambayo haijalipwa wanahimizwa kuwasiliana haraka na Msajili wa Hisa, Custody & Registrars Services Limited kupitia anwani iliyo hapa chini ili kudai migawio yao na kuepuka hatari ya migawio hiyo kuwasilishwa kwa Mamlaka.

**Custody & Registrars Services Ltd (C&R Group)**
**IKM Place, Tower B, Ghorofa ya kwanza**
**5th Ngong Avenue, Nairobi**
**Tel + 254 20 7909276**

## MABADILIKO YA UONGOZI WA BODI



**BW. JOSEPH MUGANDA**
*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Wakuu,*
*Anayeingia mamlakani*



**DKT. WILFRED KIBORO**
*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Wakuu,*
*Anayeondoka mamlakani*

### BW. JOSEPH MUGANDA AMETEULIWA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI WAKUU WA NATION MEDIA GROUP PLC

Bodi ya Wakurugenzi Wakuu wa Nation Media Group PLC inafuraha kuwatangazia kwamba Bw. Joseph Muganda ameteuliwa kuchukua hatamu ya Uenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Wakuu wa Nation Media Group PLC kutoka kwa Mwenyekiti aliyehudumu kwa muda mrefu Dkt. Wilfred Kiboro na ambaye atastaafu wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kampuni unaotarajiwa kufanyika mnamo tarehe 27, Juni 2025.

Bw. Muganda alijiunga na Bodi ya Nation Media Group PLC mnamo Novemba, 2024. Ni kiongozi mwadilifu wa kibiashara ambaye ni mtaalamu aliyebobea na mwenye tajriba ya zaidi ya miongo mitatu ya utoaji huduma bora katika mashirika mbali mbali ya kimataifa kwenye bara la Afrika na hata huko Uingereza. Majukumu yake ya awali ni pamoja na nyadhifa za daraja la juu (Mkurugenzi Mkuu Mtendaji) huko VIVO Energy Kenya (Shell Licensee), Kenya Breweries Limited pamoja na British American Tobacco, na amekuwa kiongozi wa masoko katika sekta mbali mbali. Kadhalika, alihudumu katika wadhifa wa Mkurunzi Mkuu Mtendaji kwenye shirika la Nation Media Group kati ya mwaka wa 2015 na 2018.

Bw. Muganda amehitimu kwa shahada ya Uzamili ya MBA kutoka kwa Chuo Kikuu cha Leicester na Shahada ya Masuala ya Sayansi ya B.Sc. katika Uhasibu na Usimamizi wa Kifedha kutoka Chuo Kikuu cha Buckingham. Kwa sasa, ndiye mwenyekiti wa Bodi ya Stanbic Bank Kenya na pia anahudumu katika bodi nyinginezo nyingi.

Dkt. Wilfred Kiboro atastaafu kama Mwenyekiti wa Shirika la Nation Media Group (NMG) baada ya kuhudumu kama Mkurugenzi Mkuu Asiyemtendaji kutokea Desemba 2006 na kama Mwenyekiti kuanzia 2009. Alijiunga na NMG kama Mkurugenzi Mkuu wa Nation Newspapers na baadae akawa Mkurugenzi Mkuu Mtendaji mnamo 1995, wadhifa aliohudumu hadi 2006. Katika hatamu yake, alifanya mabadiliko mengi sana yaliyobadilisha biashara kutoka kwa shirika msingi katika soko likiwa na bidhaa moja tu hadi kwa kiwango cha shirika tajika la habari lenye vitengo mbali mbali kama lilivyo kwa sasa. Hususan, aliongoza Shirika katika mkondo wa uanuai wa bidhaa ikiwa ni pamoja na utangazaji na hatimaye kupanua mbawa zake hadi Uganda na Tanzania. Aidha, alizindua mabadiliko ya safari ya kidijitali ya Shirika hili punde tu baada ya mabadiliko makubwa ya sekta ya vyombo vya habari.

Hatamu yake katika NMG imeelezewa kama iliyokuwa imejaa uwajibikaji thabiti wa uhuru wa vyombo vya habari, uadilifu wa kiuanahabari, maslahi ya umma na uwajibikaji wa kiushirika. Kadhalika, aliongoza vyema maendeleo ya ukuzaji wa vipaji katika shirika. Kama mtetezi kindakindaki wa uhuru wa vyombo vya habari, hakuchoka kupigia shime wajibu wa mashirika ya habari katika kuulingania ukweli huku akihakikisha kwamba maadili ya uanahabari bora katika shirika yanazingatiwa kuambatana na Sera za Uhariri Zilizoidhinishwa na Wenyehisa.

Bodi, Usimamizi na Wafanyikazi wa Nation Media Group PLC wanatoa shukurani zao za dhati kwa huduma na utendakazi, uwajibikaji pamoja na mchango wa Dkt. Kiboro kwenye Shirika hili. Kadhalika, wanamtakia heri njema anapostaafu pamoja na ufanisi wa mipango yake ya baadae maishani, na pia wanamkaribisha kwa moyo mkunjufu Bw. Muganda kama Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Wakuu, anayeingia mamlakani.

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi Wakuu,

Angela Namwakira
Katibu wa Kampuni
Iliyochapishwa: Tarehe 6,Juni 2025.


Nation Media Group
Media of Africa for Africa

Nation Media Group @NationMediaGrp